Je, ninaweza kupata chanjo lini?

Makundi ya watu yafuatayo yanaweza kupata chanjo ya COVID-19 hivi sasa. Piga simu kwa idara ya afya ya karibu, duka la dawa la karibu, au mtoa huduma ya afya ili uweke miadi yako. Maeneo yanayotoa chanjo yanaweza kupatikana katika https://coronavirus.utah.gov/vaccine-distribution.

- Wafanyakazi wa afya ambao wanatangamana na wagonjwa (kama vile madaktari wa meno, wataalamu wa tiba ya viungo au shughuli za kawaida, wafanyakazi wa ofisi ya mapokezi katika kliniki, udhibiti tiba, wafanyakazi wa afya ya nyumbani, nk.)
- Wafanyakazi wa muda mrefu na wakaazi wa kituo cha utunzaji
- Watoaji huduma ya kwanza kama vile wafanyakazi wa EMS, maafisa wa kutekeleza sheria, wasimamizi wa ufuatiliaji na maafisa magereza
- Mwalimu au mfanyakazi wa shule darasa la K-12
- Wakazi wa Utah walio na umri wa miaka 50 na zaidi
- Watu walio na umri wa miaka 16 au zaidi na walio na matatizo fulani yaliyo ya kiafya (angalia hapo chini)

Watu walio na umri wa miaka 16 au zaidi walio na yoyote kati ya matatizo yafuatayo ya kiafya wanastahiki chanjo ya COVID-19 (ikiwa una umri wa miaka 16 au 17, unaweza kupata chanjo ya Pfizer PEKEE):

- Ukosefu wa utendaji wa kawaida wa wengu (asplenia) ikiwa ni pamoja na watu waliotolewa wengu (splenectomy) au walio na matatizo wa wengu
- Uwiano wa Uzani na Urefu (BMI) wa 30 au zaidi
- Ugonjwa sugu wa moyo (sio shinikizo la damu) ikiwa ni pamoja na matatizo sugu ya moyo kushindwa kufanya kazi, ugonjwa wa moyo wa uzuiaji wa usambazaji wa damu kwenye tishu (ischemic), na ugonjwa sugu wa moyo wa valvu au wa kuzaliwa
- Ugonjwa sugu wa figo
- Ugonjwa sugu wa ini ikiwa ni pamoja na homa sugu ya ini B au C, ugonjwa wa ini unaosababishwa na vileo, ugonjwa wa kunyauka ini unaosababishwa na uharibifu wa mifereji ya nyongo (primary biliary cirrhosis), au ugonjwa wa ini na kibofu cha nyongo unaosababishwa na uvimbe kwenye mifereji ya nyongo (primary sclerosing cholangitis) au wingi wa chuma mwilini kupita kiasi (hemochromatosis)
- Saratani iliyotambuliwa chini ya miaka 5 iliyopita iliyoanza katika damu, uboho wa mfupa, au seli kwenye mfumo wa kinga. Aina hii ya saratani inaitwa saratani inayoanza katika damu (hematologic) (kama vile lukemia, lymphoma, na saratani ya utegili (multiple myeloma).
- Saratani iliyotambuliwa chini ya mwaka 1 uliopita ambayo haikuanzia kwenye damu au uboho wa mfupa. Aina hii ya saratani inaitwa saratani isiyotokana na damu (non-hematologic). (bila kujumuisha utambuzi wa saratani ya seli za msingi za ngozi (basal) na seli nyembamba za ngozi (squamous))
- Kisukari (Aina I au Aina II)

- Hali isiyo na kinga (kinga dhaifu) kutokana na damu, uboho wa mfupa, au upandikizaji wa kiungo; VVU; matumizi ya muda mrefu ya homoni za steroidi za kutibu magonjwa ya baridi yabisi (lcorticosteroids); au dawa zingine zinazodhoofisha kinga ya mwili
- Hali ya kinyurolojia ambayo inadhoofisha utendaji wa kupumua, ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa kupooza kwa ubongo, Down syndrome, kifafa, ugonjwa wa neva za viungo, ugonjwa wa neva za ubongo (sclerosis), hali ya myasthenia gravis, ugonjwa wa Parkinson, ugonjwa wa uharibifu wa neva (progressive cerebellar), na majeraha kwenye uti wa mgongo (lquadriplegia) au kupooza kwa upande mmoja wa mwili (hemiplegia)
- Wanaopokea uchepushaji njia ya mkono kutokana na ugonjwa sugu wa figo
- Wanaopokea tiba ya kukandamiza kinga
- Ugonjwa wa selimundu
- Ugonjwa sugu wa kupumua (isipokuwa pumu) ikiwa ni pamoja na ugonjwa sugu wa mapafu unaozuiwa kusambaa kwa hewa (obstructive pulmonary), ugonjwa wa uharibifu wa tishu za mapafu (fibrosing lung disease), ugonjwa wa uharibifu kabisa wa mirija ya hewa (bronchiectasis), au ugonjwa wa kurithi unaosababisha vimiminika vilivyo ndani ya mwili kuwa vizito na kunata (cystic fibrosis)
- Mpokeaji wa upandikizaji wa kiungo
- Kiharusi na ulemavu wa akili (Alzheimer's, uharibifu wa ubongo kutokana na matatizo ya usambazaji wa damu (lvascular), au matatizo ya sehemu ya mbele ya ubongo (frontotemporal)

Huna haja ya kuwa na nyaraka ya daktari ili kuweka miadi ya chanjo yako.

Wagonjwa ambao hawatimizi vigezo hivi wanahitaji kusubiri hadi wale walio katika hatari zaidi wapate chanjo. Tunatambua kuwa kuna hali nje ya orodha hii ambazo ziko katika hatari kubwa pia; Hata hivyo, tuna chanjo za kutosha tu kwa wale wanaostahiki kupitia hali hizi hivi sasa. Watu hawa wako katika hatari kubwa ya kulazwa hospitalini na kufariki kutokana na COVID-19 na tunahitaji kuhakikisha wamepata chanjo haraka iwezekanavyo.

Ni nani atakayefuata?

Tunatarajia chanjo za COVID-19 zitapatikana kuanzia Aprili kwa vikundi vingine vya umri, watu walio na hali ya kimatibabu ambayo haijaorodheshwa hapo juu, na wale ambao wanaishi katika mazingira yenye watu wengi na wako katika hatari kubwa ya kuathiriwa na virusi vinavyosababisha COVID-19. Chanjo zinapaswa kupatikana kwa umma mwishoni mwa msimu wa kuchipua au mapema msimu wa kiangazi.

Hauhitaji "kuwa kwenye orodha ya wanaosubiri" ili upate chanjo. Chanjo itakapopatikana, tunatarajia kuitoa katika maeneo mengi katika jamii yako. Maeneo haya yatachapishwa katika https://vaccinefinder.org/.